

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

Anuani ya Simu: "TAMISEMI"
Simu Na: (026) 2322848, 2321607
2322853, 2322420
Nukushi: (026) 2322116, 2322146
2321013
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz



Tawala za MKOA na
Serikali za Mitaa,
Jengo la Mkapa,
2 Barabara ya hospitali,
S.L.P. 1923,
41185 DODOMA.

TANGAZO LA KUITWA KAZINI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) kwa kushirikiana na Taasisi ya Benjamin Mkapa pamoja kwa kupitia mradi wa Mfuko wa Dunia wa kupambana na magonjwa ya Kifua Kikuu, Malaria na HIV/AIDS (GFATM) na Mradi wa Mkapa Fellows Program Awamu ya Tatu, inapenda kuwataarifu waombaji wote waliomba nafasi mbalimbali za kazi kuanzia tarehe **09 Mei, 2018** hadi tarehe **25 Mei, 2018** kupitia OR - TAMISEMI kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi kwa awamu ya pili umekamilika hivyo mnatakiwa kuripoti katika vituo vyenu vya kazi.

Watumishi wote waliopangiwa vituo vya kazi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo: -

- i) Kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa kuanzia tarehe 27/09/2018. Aidha waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi kwa tarehe hiyo bila ya taarifa, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.
- ii) Kuwasilisha kwa waajiri wao vyeti halisi (**Originals Certificates**) vya masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea kwa ajili ya kuhakikiwa na waajiri kabla ya kupewa barua za ajira.
- iii) Kuwasilisha cheti cha usajili/leseni, cheti cha mazoezi kwa vitendo (internship) kwa kada zinazohusika kama vile; madaktari, wafamasia, wateknolojia na wauguzi.

- iv) Picha mbili (2) – saizi ya Pasipoti na maelezo binafsi (CV), ikionyesha umri, anuani kamili ya Posta na barua pepe na namba ya simu ya kiganjani, pamoja na anuani/ namba ya kiganjani ya wadhamini wako wasiopungua watatu (3).
- v) Hakutakuwa na mabadiliko ya vituo, watakaoshindwa kuripoti katika muda uliopangwa, nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo.

Orodha ya majina ya watumishi wote waliopangiwa vituo vya kazi yanapatikama kupitia tovuti ya OR - TAMISEMI www.tamisemi.go.tz.
na Benjamin Mkapa Foundation www.mkapafoundation.or.tz.

- Aidha tunapenda kuwafahamisha wote waliopangiwa kuwa, ajira hizi ni za mkataba na zinasimamiwa na Taasisi ya Mkapa kupitia mradi wa Global Fund na Mradi wa Mkapa Fellows Awamu ya Tatu. Na pia tunapenda kuwafahamisha kuwa pamoja na kuwa kwamba ajira hii ni ya mkataba, kabla au baada ya kukamilika kipindi cha mkataba, waajiriwa wote katika miradi tajwa **watapata nafasi ya** kujiunga katika Utumishi wa Umma kulingana na taratibu za Serikali za Ajira iwapo kibali cha ajira kitakapopatikana.

Wale wote waliochaguliwa, wanombwa kutoa taarifa ya ukubali wao ndani ya siku saba kupitia barua pepe kwa address ya info@mkapafoundation.or.tz na kisha kuripoti katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa mikoa waliyoyopangiwa asubuhi saa 2:30 kwa ajili ya taratibu nyingine za ajira kama ilivyoainishwa katika jedwali na 1: -

Jedwali na 1: Ratiba ya awali kuhusu mafunzo elekezi

NA	MKOA	MAHALI	TAREHE	MUDA
1	Tabora	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	27/09/2018	2:30 asu - 8 mch
	Katavi	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	28/09/2018	2:30 asu - 8 mch

NA	MKOA	MAHALI	TAREHE	MUDA
	Kigoma	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	29/09/2018	2:30 asu - 8 mch
	Dodoma	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	30/09/2018	2:30 asu - 8 mch
2	Simiyu	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	27/09/2018	2:30 asu - 8 mch
	Geita	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	28/09/2018	2:30 asu - 8 mch
	Kagera	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	29/09/2018	2:30 asu - 8 mch
3	Shinyanga	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	27/09/2018	2:30 asu - 8 mch
	Mwanza	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	28/09/2018	2:30 asu - 8 mch
	Mara	Ofisi ya Mkuu wa Mkoa	29/09/2018	2:30 asu - 8 mch

Limetolewa na:-

OR - TAMISEMI kwa ushirikiano na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Mkapa

14/09/2018

